Kufumba na kufumbua, pu! Mlango ulipigwa teke na kuanguka kando. Mlangoni walisimama maafisa wanne wa polisi na bastola huku wawili wakiwa na pingu mikononi. Mlaraha aliinua mikono juu ishara ya kusalimu amri. Moyoni alijua kuwa zake arubaini zilikuwa zimetimia. Naam, uhalifu haulipi chochote.

121. Mlaraha hakuweza kuiwahi rununu yake kwa kuwa
   A. kichwa chake kilikuwa kizito.
   B. ilikuwa mbali.
   C. hakutaka kufanya hivyo.
   D. aliogopa kuzungumza na aliyekuwa akipiga.

122. Chagua orodha ya sifa za Mlaraha kulingana na kifungu.
   A. Mwizi, mpole.
   B. Mlevi, mwizi.
   C. Mjeuri, mlevi.
   D. Mwizi, katili.

123. Ni kweli kuwa waliobisha mlango walikuwa
   A. wenzake Mlaraha katika wizi.
   B. majirani waliotaka kumjulia hali Miaraha.
   C. maafisa wa polisi.
   D. waumini wa dhehebu aliloshiriki.

124. Methali gani inayoweza kutumika kufupishia kisa hiki?
   A. Pwagu hupata pwaguzi.
   B. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.
   C. Kawia ufike.
   D. Siku za mwizi ni arubaini.

**<u>Sema kifungu kifuatacho kisha ulibu maswoll 125 hadi 127</u>**

Uhalifu ni hali ya kutenda kinyume na zinavyohitaji sheria za nchi ambazo siku zote huongozwa na katiba. Kunavyo viwango mbalimbali vya uhalifu katika jamii. Uhalifu hutendeka katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, kuna njia kadhaa za kukabiliana na uhalifu. Kwanza, wananchi wakiacha tabia za kuwaficha wahalifu miongoni mwao, uhalifu utapungua. Vile vile, wale

ambao hupokea hongo wanastahili kufunguliwa mashtaka. Si hayo tu, uhalifu aidha huweza kupungua iwapo sehemu mbalimbali za umma kama vile afisini zitawekewa kamera za siri. Kwa jumla, kila mwanajamii akisimama kidete kupambana na uhalifu, tutaweza kujivunia kupungua kwa uhalifu.

125. Mwandishi ametaja njia ngapi za kukabiliana na uhalifu?
   A. Tano.
   B. Nne
   C. Mbili.
   D. Tatu.
126. Kulingana na habari hii, kamera za siri zinaweza kudhibiti uhalifu
   A. nyumbani.
   B. afisini.
   C. shuleni
   D. sokoni.
127. Kwa jumla, jukumu la kudhibiti uhalifu ni jukumu la nani?
   A. Serikali.
   B. Watu wazima.
   C. Kila mmoja.
   D. Wazazi.

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 128 hadi 130.</u>**

Shughuli kama vile kuogelea, kandanda, riadha na urukaji viunzi huitwa michezo. Shughuli hizi si muhimu tu katika kuijenga miili yetu bali pia huchangia kuwaleta watu pamoja. Michezo baina ya shule mbalimbali huwaleta wanafunzi pamoja ambapo wao huweza kubadilishana mawazo yanayoweza kuinua viwango vyao vya kimasomo. Shughuli za kimichezo aidha huchangia kutukinga dhidi ya magonjwa kama vile uzito wa mwili, ambayo hatimaye huweza kusababisha maradhi ya moyo. Baadhi ya wananchi hutumia michezo kama kitegauchumi cha kuwaletea pesa. Baadhi ya wanaspoti wamewahi kuiletea nchi yetu nishani na medali mbalimbali na hivyo kuiweka nchi yetu katika nafasi bora kimichezo.

128. Chagua kauli isiyo sahihi kulingana na ufahamu.
   A. Shughuli za kimichezo si muhimu katika kuijenga miili yetu.
   B. Michezo haichangii katika kujenga miili yetu pekee.
   C. Wakati mwingine michezo huandaliwa baina ya shule mbalimbali.
   D. Baadhi ya watu hutumia michezo kama njia ya kujipatia riziki.
129. Kulingana na habari hii, uzito wa mwili hatimaye huweza kusababisha
   A. mauti.
   B. uvivu.
   C. maradhi ya ngozi.
   D. maradhi ya moyo.
130. Nchi yetu inapopata nishani na medali,

A. wananchi wengi hujiunga na spoti.
B. hadhi yake kimichezo huinuka.
C. hupoteza heshima yake kimichezo
D. huwa miongoni mwa mataifa yaliyotajirika.

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 131-135.**

(*Mwalimu na wanafunzi wamo katika mjadala kuhusu umuhimu wa kuyatunza mazingira*)
Bi Muli: Salaam aleikum wanafunzi. M hali gani?
Wanafunzi: (*Wakiamka sawia*) Njema Bi Muli, shikamoo.
Bi. Muli: Marahaba (*anawaashiria wakae*) Naam, leo ningependa tuzungumze kuhusu namna n umuhimu wa kuyatunza mazingira kwa kuwa mazingira machafu huweza kutuletea magonjwa hatari.
Sofa: Samahani mwalimu, mazingara ni nini? (*Akionyesha uso wa kuchanganyikiwa*)
Bi Muli: Sofia, si mazingara, ni mazingira. Haya ni yote ambayo...
Peru: (*Akiunyanyua mkono wake*) Samahani mwalimu, naweza kulijibu swali hilo. Haya ni yote ambayo yanatuzunguka.
Bi Muli: Makofi kwa Peru. (Wenzake wanampigia makofi kwa kujibu swali kwa usahihi). Safi. Ili kuyalinda mazingira, tunaweza kukata nyasi ndefu zinazowafuga mbu.
Maloba: Vile vile, tunaweza kuhakikisha vyanzo vya maji vi safi. Hivi ni kama vile mito, maziwa na mabwawa.
Ali: Nadhani kuwa kuna hatari aidha katika kutumia mbolea za madukani kiholela. Zikitumiwa kupita kiasi huweza kuathiri udongo na hatimaye vyanzo vya maji.
Bi Muli: Vyanzo vya maji vinapoathirika, viumbe vya majini kama vile samaki, mamba, mimea na wanyama wengine huweza kuathirika pakubwa. Kesho tutaandika insha kuhusu umuhimu wa kuyatunza mazingira. Kwaherini kwa sasa.
Wote: Kwaheri ya kuonana mwalimu.

131. Kulingana na maelezo ya mwalimu, mazingira machafu yana madhara gani? Huweza
   A. kuchafua vyanzo vya maji.
   B. kusababisha magonjwa.
   C. kudumisha afya bora.
   D. kutukinga dhidi ya magonjwa.
132. Peru alipigiwa makofi kwa sababu
   A. alilijibu swali la mwanafunzi mwenzake kwa usahihi.
   B. alikuwa mwanafunzi bora darasani mwao.
   C. alijaribu kulijibu swali la Sofia.
   D. alishindwa kulijibu swali la Sofia.
133. Kulingana na mazungumzo haya, mbolea za madukani zikitumika kupita kiasi
   A. huweza kusababisha hali mbaya ya anga.
   B. huweza kuchafua hewa.
   C. huathiri udongo na vyanzo vya maji.
   D. huchafua pakubwa vyanzo vya maji

134. Vyanzo vya maji vínapoathirika,
    A. wanyama wa porini huangamia.
    B. nyuni wa angani hufa.
    C. wanadamu hupata taabu.
    D. wanyama wa majini huathirika.
135. Chanzo gani cha maji hakijatajwa katika mazungumzo haya?
    A. Mito.
    B. Mvua.
    C. Mabwawa.
    D. Maziwa.

**Soma kifungu kifuatacho. Chagua jibu lifaalo zaidi kati va vale uliyopewa.**

Mtoto ana haki ___136___. Yapo inahitaji ya kimsingi ambayo ni makazi, lishe na ___137___ haki ya mtoto kupata elimu___138___serikali ikaanzisha elimu ya bure katika shule za umma.___139___ anayemnyima intoto nafasi ya___140___shuleni lazima afikishwe mahakamani.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 136. | mingi | chache | zote | kadhaa |
| 137. | elimu | makao | mavazi | maji |
| 138. | sababu | maana | ili | ndipo |
| 139. | Wowote | Yeyote | Yoyote | Wote |
| 140. | kuenda | kufika | kusomesha | kuanguka |

**Kutoka swali la 141-150. jibu swall kulingana na maagizo uliyopewa.**

141. Chagua kitenzi kilicholinganishwa visivyo na kinyume chake.
    A. Funga fungua
    B. Shona shonua
    C. Nuna tabasamu
    C. Lia cheka
142. Kamilisha tashbihi hii:
    **Mariamu ana maneno mengi kama**
    A. chiriku.
    B. tausi.
    C. kasuku.
    D. njiwa.

143.Chagua ukubwa ws:

**Ndizi hizi ni ndogo.**

A. Dizi hili ni dogo.
B. Kidizi hiki ni kidogo.
C. Madizi haya ni madogo.
D. Vidizi hivi ni vidogo.

144.Chagua ukanusho wa sentensi ifuatayo:

**Wewe ulikuwa mgonjwa.**

A. Wewe haukuwa mgonjwa.
B. Wewe hujawa mgonjwa.
C. Wewe huwi mgonjwa.
D. Wewe hukuwa mgonjwa.

145.Chagua sentensi iliyo katika hali timifu.

A. Mboso atauimba wimbo mpya.
B. Kadogo amemaliza kuandika.
C. Upepo haukuvuma kwa fujo.
D. Walimu wanazungumza mkutanoni.

146.Chagua wingi wa sentensi ifuatayo:

**Ufagio ulinunuliwa sokoni.**

A. Fagio zilinunuliwa masokoni.
B. Ufagio zilinunuliwa sokoni.
C. Fagio ulinunuliwa masokoni.
D. Ufagio ulinunuliwa masokoni.

147.Chagua orodha ya nomino zilizo katika ngeli tofauti.

A. Cheo, chupa.
B. Magari, maua.
C. Kiwavi, kipofu.
D. Mitego, mikoba.

148.Ni sentensi gani iliyo katika nafsi ya pili?

A. Mlitutembelea jana kwa sherehe.
B. Alinunuliwa mwanasesere maridadi.
C. Nimeamua kufanya bidii.
D. Mwalimu aliyekuwa darasani ametoka.

149.Chagua methali iliyo tofauti na nyingine kimatumizi.

A. Kidole kimoja hakivunji chawa.
B. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.
C. Mkono mmoja haumlei mwana.
D. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.

150.Chagua orodha ya majina ambayo ni visawe.

A. Runinga, redio
B. Ndovu, Pombe
C. Mbung'o, ndorobo
D. Ugonjwa, malaria

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 151-155.**

(Mchezaji wa kabumbu amekutana na mkufunzi wake. Wanajadiliana kuhusu hali ya mchezaji.)

**Kocha :** Vipi kaka? Habari za asubuhi? Waonekana kuchechemea. Kulikoni? (akionyesha mshangao mkuu)
**Mchezaji:** Habari nzuri ila si sana. Ni kweli, nachechemea kutokana na maumivu ya goti langu la kushoto. Nadhani unakumbuka kilichotokea katika uwanja wa Mwagajasho tulipocheza dhidi ya timu ya Majimoto.
**Kocha :** Naam, nakumbuka ulichezewa visivyo ikakubidi kuuaga mchezo. Nilidhani ulipata nafuu. Je, umepokea matibabu yoyote hadi sasa?(alimgusa na kumpapasa gotini)
**Mchezaji:** Naam, bata sasa nimetoka kupokea huduma pale hospitalini Dawatamu. Daktari Siha amenishauri kuufanyisha mazoezi mguu huu ili goti lipone upesi. (akiukunja na kuunyosha mguu wake wa kushoto)
**Kocha** : Nakutakia afueni ya haraka bwana Kadenge. Kumbuka kuwa tutakuwa na mechi kali dhidi ya timu ya Wazee Hukumbuka wiki ijayo. Mchezaji: Aa! Nitakuwa nimepona kocha. Asante sana kwa kunikumbusha.
**Kocha :** Hewallah bwanamogo. Tutaonana wakati mwingine majaliwa

151.Hali ya mchezaji ilikuwa shwari ila
A. viungo vyake.
B. miguu yake
C. magoti yake.
D. goti lake

152.Je, ni nini kinatueleza kuwa mkufunzi alimjali mchezaji wake?
A. Alimkumbusha mchezaji kuhusu mechi iliyokaribia.
B. Alimshughulikia mchezaji wake vilivyo kimatibabu.
C. Alitaka kufahamu sababu ya mchezaji kuchechemea.
D. Alimsaidia mchezaji kunufanyisha mgw mazoezi.

153.Kulingana na bwana Siba, mazoezi ya Kadenge ni nani?
A. Yule mchezaji aliyeumia wakati wa mechi.
B. Mkufunzi wa mchezaji yule.
C. Mwuguzi katika hospitali ya Dawatamu.
D. Daktari katika hospitali ya Dawatamu.

154.Je, kocha alipokutana na mchezaji huyo alikuwa ametoka wapi?
A. Hospitalini Dawatamu.
B. Hatujaelezwa.
C. Kwa daktari. '
D. Uwanjani.

155.Kulingana na mazungumzo haya, mara kwa mara yalikuwa na umuhimu gani?
A. Yangemwongeza mchezaji nguvu
B. Ili mchezaji awe imara.

C. Yangeiponya miguu ya mchezaji .
D. Yangeharakisha kupona kwa goti la mchezaji.

**Soma kifungu kifuatacho kisha wilbu maswali 156 hadi 158.**

Katika enzi za kale, watu hawakuwa wakivaa nguo zozote. Wacheshi husema kuwa walivalia suti ya Mungu! Miaka ilivyozidi kubingirika, watu wakaona umuhimu wa kujisitiri . Hapo, wakaanza kujifunika kwa ngozi za wanyama. Baadaye, walianza kutumia mablanketi na mashuka.

Leo hii tumapozungumza, kuna aina nyingi sana za mavazi kiasi kuwa ni vigumu kuchagua ya kimunua. Kama ilivyo kawaida, watu hutofautiana katika chaguzi za aina na rangi za mavazi. Yapo mavazi ambayo ni ya wanaume pekee. Vilevile, kunayo yale ambayo ni ya wanawake tu. Baadhi ya haya ya kike ni kanchiri au sidiria, marinda, sketi, blauzi na mengineyo. Watoto nao hawajaachwa nima Yapo mavazi ambayo ni ya watoto tu. Je, wafahamu kuwa kuna mavazi yanayoweza kuvaliwa na wanawake na pia wanaume?

156.Kulingana na taarifa,
A. zamani watu walivalia mavazi ya bei rahisi.
B. hakukuwa na nguo zozote kitambo.
C. kitambo, watu walikuwa na tatizo la kuchagua nguo za kununua.
D. watu walijisitiri kwa majani mapana

157.Ni jibu gani laonyesha hatua alizopitia binadamu hadi kuufunika mwili wake?
A. Mablanketi na mashuka, mavazi, ngozi za wanyama.
B. Mavazi, mablanketi na mashuka, ngozi za wanyama.
C. Ngozi za wanyama, mablanketi na mashuka, mavazi.
D. Mablanketi na mashuka, mavazi, ngozi za wanyama.

158.Kulingana na ufahamu huu, watu wa sasa tatizo gani kuhusiana na nguo?
A. Nguo zilizopo hazimtoshelezi kila mmoja.
B. Wingi wa aina za mavazi hufanya kuchagua kuwe kungumu.
C. Mavazi mengi ya kisasa ni ya wanawake na wanaume.
D. Kunayo mavazi ya wanaume, wanawake na watoto.

159.Baadhi ya mavazi ya wanawake katika kifungu ni ana
A. marinda, sidiria na blauzi.
B. sketi, chupi na kanchiri.
C. suruali, marinda na sidiria.
D. kanchiri, tai na sketi.

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 160 hadi 162.**

"Wageni wetu waheshimiwa, wazazi, walimu, wakufunzi wa michezo, wachezaji na wanafunzi wenzangu, habari za wakati huu? Hakika, bila kubahatisha maneno, leo ni siku muhimu sana katika tukio ya humu shuleni ya mwaka huu. Naam, ni siku ya kutiwa katika rekodi ya kumbukumbu ili isisahaulike na yeyote. Kama tujuavyo sote, michezo ni njia

mojawapo ya kuonyesha uwezo na alanta alizotujalia Mwenyezi Mungu. Naomba nigusie faida kadhaa za michezo. Michezo huipa miili yetu na kutufanya tuwe na afya bora. Kupitia michezo, uwezo wetu wa kushiriki vyema katika timu huonekana. Viungo vyetu hufanya kazi vizuri, uhusiano wetu na wenzetu hujengeka na mawasiliano miongoni mwetu huwa bora. Kujihusisha na michezo baada ya kazi za darasani na nyumbani hupumzisha akili. Tunapojiandaa kushiriki mchuano wa leo, nawatakia kila la heri. Asanteni kwa kunisikiliza."

160.Unadhani aliyetoa maelezo haya alikuwa napi?
   A. Mzazi.
   B. Mwalimu
   C. Mwanafunzi.
   D. Mchezaji.

161.Ni gani hapa si umuhimu wa michezo
   A. kulingana na kifungu hiki?
   B. Miili yetu hupata nguvu na kutufanya tuwe na afya bora.
   C. Baadhi ya magonjwa hutuondoka miilini tukishiriki michezo.
   D. Uhusiano baina yetu na wenzetu huimarika.

162.Michezo huleta pumziko la akili baada ya shughuli fulani ngumu.
   A. Kuna uwezakano kuwa siku hiyo ilikuwa ya
   B. kuwatakia wachezaji kila la kheri.
   C. kufungwa rasmi kwa shule.
   D. kuzawidiwa kwa wachezaji bora
   E. michezo shuleni humo.

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha vilbu maswali 163 hadi 165.</u>**

Kila Jumamosi, mama huenda katika soko la Marikiti ili kuuza bidhaa zake. Yeye huruza matunda ya aina nyingi kama mapapai, maparachichi, maembe, mananasi, machungwa na makarakara. Vile vile, huuza mboga kama kabeji, mchicha na sukumawiki. Aliacha kuuza nyanya na vitungw baada ya bidhaa hizo kuwa ghali zaidi katika soko kuu.

Mimi ndimi mwanambee katika familia yetu, hivyo, mama huniachia majukumu kila aondokapo. Kaka zangu wawili na dada zangu watatu hunisaidia kufanya kazi pale nyumbani.

Jumamosi iliyopita, mama aliondoka kwenda sokoni kama ilivyokuwa kawaida. Tuliamua kugawana kazi pale nyumbani ili tuzimalize kabla hajarejea kutoka sokoni. Niliwaambia dada zangu Wafue, wasafishe nyumba na kupika kishuka. Kaka zangu walitakiwa kufyeka nyasi, kuulengata ua na kuchoma taka. Ghafla, niliskia mlio wa mbuzi wetu. “Ni nani atakayewapeleka mbuzi malishoni?" Nikajiuliza.

163.Familia ya kina mwandishi ina jumla ya watu wangapi?
   A. Saba
   B. Sita.
   C. Wanane.
   D. Watano.

164. Ni kwa nini mama wa mwandishi hauzi nyanya na vitunguu?
   A. Bidhaa hizo hazipatikani katika soko kuu.
   B. Bei ya bidhaa hizo imepanda mno katika soko la Marikiti.
   C. Bidhaa hizo zimekuwa ghali mno katika soko kuu.
   D. Nyanya na vitunguu hazipatikani katika soko la Marikiti.
165. Chagua orodha ya bidhaa ambazo mama wa mwandishi huuza.
   A. Karoti, mboga na nyanya.
   B. Kabeji, matunda na vitunguu.
   C. Mayai, matunda na mboga.
   D. Kabeji, makarakara na maembe.

**Soma kifungu kifuatacho. Chagua libu taalo zaidi kati ya yale uliyopewa**

Uchaguzi uliokamilika hivi majuzi ulidhihirisha kuwa, kwa sasa, wananchi ni wapenda amani. Wengi walidhani kuwa, baada ya mshindi wa __166__ urais kutangazwa, wakenya wangetafuta silaha za kutoana __167__ na kuharibiana mali. Kinyume na hivyo, amani __168__ kote. Huu ndio moyo wa uzalendo. Tukubali matokeo na tuendelee kufanya kazi ili kuboresha __169__ Ni kweli barwa asiyekubali kushindwa __170__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 166 | A. meza ya | B. dawati la | C. kiti cha | D. kabati la |
| 167 | A. mamlakani | B. roho | C. ofisini | D. mikono |
| 168 | A. imetamalaki | B. imepungua | C. imezorota | D. imepotea |
| 169 | A. uhuru | B. umaskini | C. utawala | D. uchumi |
| 170 | A. ni mshindi | B. si mshindani | C. si mshindaji | D. ni mshindani |

**Katika swali la 171 - 180, jibu swall kulingana na maagizo uliyopewa**.

171. Ni sentensi gani haijatumia **amba** kwa usahihi?
   A. Maua arabayo walichuma yananukia.
   B. Wageni ambao walingojewa walifika.
   C. Majina ambao walitajiwa hayakiwa yao.
   D. Masomo ambayo tulisomeshwa yalitufaa.

172. Chagua neno lililo katika ngeli tofauti.
   A. Mezani.
   B. Mfukoni.
   C. Sahani.
   D. Chumbani.
173. Chagua sentensi iliyo katika kauli ya kutendesha..
   A. Tiko na kosa huandikiana barua.
   B. Rama ameufunga mlango.

C. Mzee Tomoko amepanda miche.
D. Mvua kubwa ilikatiza safari

174. Ni mnyama yupi hapa baishi majini?
A. Samaki.
B. Kuchakulo.
C. Mamba
D. Kiboko

175. Tumia kiámbishingeli sahihi kukamilishia sentensi ifuatayo:
Hatuku la uyoga wenye sumu.
A. U
B. ya
C. i
D. zi

176. Chagua wingi wa sentensi ifuatayo: Maji yaliyotekwa yamemwagika.
Maji
A. zilizotekwa zimemwagika.
B. yaliyotekwa yamemwagika.
C. iliyotekwa imemwagika.
D. waliyoteka yamemwagika.

177. Kamilisha methali ifuatayo: Kidole kimoja
A. hujaza kibaba
B. walaji ni wengi.
C. huvikwa pete.
D. hakivunji chawa.

178. Ni sentensi ipi haijatumia kivumishi kimilikishi kwa usahihi?
A. Jirani yangu anaitwa Tindi.
B. Madarasa yao yameoshwa vizuri.
C. Kina mama yao wana mioyo safi.
D. Mjomba wetu hapendi kununa.

179. Chagua majina yaliyo katika ngeli ya A-WA.
A. Uzi,
B. Kuta, nyuzi, ufizi.
C. Nzi, kipepeo, kiroboto.
D. Utepe, uteo, uchafu.

180. Chagua sentensi iliyoakifishwa kwa usahihi.
A. Wanyama wafugwao ni pamoja na: ngo'mbe, mbuzi na kondoo.
B. Ukienda, ng'ambo uniletec haya: vikoi, saa na mkufu.
C. Ala, kumbe unajua kuendesha baiskeli.
D. Mwalimu alisema tulete nini kesho.

**<u>Soma mzungumzo yafuatayo kishu ujibu maswali 181-184</u>**

Jona: Shikamoo dada? Umetulia sana hapa jikoni. Unafanya nini?
Hadija: Marahaba ndugu yangu. Nataka nimalize kuosha vyombo. Ningependa kumrahisishia mama kazi atakapokuja kuandaa chajio.
Jona: Huo ni uamuzi wa busara. Hebu nikusaidie ili tumalize kazi hiyo nawe ukafanye kazi ulizopewa shuleni.
Hadija: (Akitabasamu) Asante. Naona unaelewa kuwa kinga na kinga ndipo moto liwakapo.
Jona: (Huku ukizichukia suhuni azioshe kwenye kuro) Wajua ni jukumu letu kuwasaidia wazazi hapa nyumbani. Huu ndio mchango wetu katika kupunguza matumizi. Au wasemaje dada?
Hadija: Kweli kabisa. Hapo umegonga ndipo. Hakuna haja ya wazazi kuwaajiri vijakazi na vitwana wafanye kazi za nyumbani ilhali mzazi ana watoto wakubwa kama sisi.
Jona: Maadamu tumeimaliza shughuli ya usafi naomba uje unielekeze kufanya hesabu mbili zinazonitatiza.
Hadija: Hlewala, nitakusaidia.
Jona: Asante dada. Tahika ndugu ni kufaana, si kufanana.

181.Mazungumzo haya yanaonyesha kuwa
   A. Jona ni mkubwa kuliko Hladija.
   B. Tadija ni mkubwa kuliko Jona.
   C. Hadija ni mkubwa kuliko Jona.
   D. Jona ni mwerevu kuliko Hadija.

182.Watoto hawa ni wenye busara kwa sababu,
   A. wanajua umuhimu wa kuwasaidia wazazi.
   B. wanafanya kazi za nyumbani badala ya kusoma.
   C. wanafahamu ubaya wa vijakazi na . vitwana.
   D. wanaogopa kugombezwa na wazazi wao.

183.Usemi hapo umegonga ndipo' una maana. kwamba
   A. aliyosema Jona si kweli.
   B. aliyosema Jona hayawezekani.
   C. aliyosema Jona yanashangaza.
   D. aliyosema Jona ni ukweli.

184.Umuhimu wa ndugu kulingana na mazungumzo ni
   A. kuishi pamoja.
   B. kupeana msaada.
   C. kufanana sana.
   D. kufanya hesabu.

**<u>Soma kifungu kifuatacho kishú ujibu muswali 185 - 188</u>**

Kobe alikuwa akitoka **cheteni** kuuza mboga zake. Siku hiyo, mboga zilinunuliwa zote hata akahitajika kupeleka zaidi. Wateja wake walifurahishwa na mboga zake maadamu hakutumia kemikali zenya madhara. Hakutaka wale waliotumia mboga hizo wadhurike.

Njiani, alikutana na Pundamilia na Ngiri. Aliwasaili kuhusu walikokuwa wakitoka

wakati ule. Pundamilia alimjibu, "Tumetoka kupanda miti upande wa mashariki wa msitu huu. Tumegundua kuwa binadamu ameikata miti mingi sana. Hali hii akiendelea kutatokea kiangazi." Kobe aliwashukuru na kuwapongeza wenzake kwa uamuzi wao wa busara. Kisha akasema, "Hakika mtego wa panya huingia waliokuwemo na wasiokuwemo. Ni muhimu tuzuje hatari ya ukosefu wa mvua kwa kupanda miti. Nitaenda huko kesho nitimize wajibu wangu."

Baada ya hapo, wanyama wale walipungiana mikono, Kobe akajiendea zake. Akilini aliwaza, "kwa nini binadamu hatumii akili yake razini? Tamaa hii ya kukata miti kwa kutaka utajiri wa haraka, si itamwangamiza? Isitoshe, juzi nilipopita karibu na kijiji chao, niliona wamerundika taka kila mahali. Hakika wasipoubadili mkondo huo watajuta baada ya kuathirika."

185. Neno jingine lenye maana sawa na cheteni ni
   A. sokoni
   B. nyumbani
   C. shambani
   D. mjini
186. Kwa nini wateja walizipenda mboga za Kobe? Kobe
   A. alikuwa rafiki wa kila mtu.
   B. alikuwa mkulima hodari.
   C. alijali afya ya wateja wake.
   D. aliziuza kwa bei nafuu.
187. Ahadi aliyotoa Kobe ni kuwa,
   A. A. angezuia uharibifu wa msitu wao.
   B. angeenda kupanda miti siku iliyofuata.
   C. angemshauri binadamu aache kuharibu mazingira.
   D. angeenda kupeleka mboga upande wa mashariki.
188. Tabia za binadamu zinazokashifiwa na Kobe ni
   A. uchoyo na uharibifu.
   B. ukatili na uvivu.
   C. mapuuza na kujitenga.
   D. tamaa na uharibifu.

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 189 - 192.**
(Sunkuli na Malaika wamekutana njiani)

Sunkuli: Habari rafiki yangu?
Malaika: Nzuri mwenzangu sunkuli. Je, safari ya wapi jioni hii?
Sunkuli: Naenda kwa Mama Fatuma kumpekelekea chakula. Amekuwa akiugua tangu juzi. Mama amenituma nikamjulie hali na kumpa maziwa haya
Malaika: Ooh! Bi Fatuma yuaugua. Kumbe ndiposa sijamwona akipita karibu na kwetu hivi karibuni. Wajua hawezi kupita bila kutoa salamu.
Sunkuli: Kwa hakika Bi Fatuma ni mtu wa watu. Watu wote wangemwiga yeye, taifa lingekuwa na mshikamano mzuri sana. Maovu mengi yangeisha kwani kila mtu angemchukulia mwenzake

kama ndugu.
Malaika: Haya ukifika kwa Bi Fatuma umpe salamu zangu. Nitaenda kumjulisha mama kuhusu maradhi yake. Nikipata kibali nitaenda kuzuru kesho mwendo wa adhuhuri.
Sunkuli: Sawa Malaika. Nina uhakika kuwa utapewa idhini hiyo. Wema hauozi. Hakuna mtu anayeweza kumnyima Bi. Fatuma msaada.
Malaika: Haya, hebu nenda usije kuchelewa. Kwaheri.
Sunkuli: Kwaheri na uwe na jioni njema,

189. Sunkuli alipokutana na Malaika alikuwa,
   A. akitoka kumsaidia Bi Fatuma.:
   B. ameenda kuona kama Bi Fatuma aliugua.
   C. ameenda kumjulia hali Bi Fatuma.
   D. ametoka kuchukua maziwa kwa Bi Fatuma.
190. Neno ooh! ni aina ya
   A. kielekezi
   B. kiingizi
   C. kihusishi
   D. kiwakilishi.
191. Bi Fatuma ni mtu wa watu ndiko kusema,
   A. anajulikana na watu wengi.
   B. anasaidiwa na watu wengi.
   C. amewasaidia watu wote.
   D. anahusiana vyema na watu.
192. Malaika anaahidi kuenda kumsaidia Bi fatuma. Msaada huu utatolewa ikiwa
   A. atapewa ruhusa.
   B. atapata wakati
   C. hatakuwa amepona.
   D. hatakuwa na kazi nyingine.

**Soma kifungu kifuatacho kisha uyajibu maswali 193 - 195**

Shawe alikuwa na mazoea ya kuenda msalani mara kwa mara kwa haja ndogo. Mwalimu wake aligundua jambo hilo. Alimwita mlezi wake ofisini mwake. “Asante kwa kuitikia mwito wangu, Naomba umpeleke mwana wako kwenye hospitali achunguzwe," Mwalimu akasema.
Shawe alipelekwa hospitalini kwanza alipimwa uzani wake. Baada ya kadi yao ya matibabu kukaguliwa, walitumwa maabarani. Damu yake ilifanyiwa vipimo. Daktari alimwuliza maswali kadhaa. “Daktari, kibofu changu hujaa haraka nami hushindwa kustahimili,” Shawe alimwambia tabibu. Shawe alipigwa picha ya eksirei. Picha hiyo ilionyesha kuwa mafigo yake yalikuwa na tatizo. Kwa bahati nzuri tatizo liligunduliwa mapema. Alipendekezwa kulazwa hospitalini ili atibiwe himahima. Ndugu zake, majirani na wanafunzi wenzake walimwombea apate afueni.

193. Jambo linaloonyesha kuwa Shawe alikuwa na shida ni kwamba
   A. mwalimu alimwita mlezi wake shuleni.

B. alikuwa akienda msalani mara mojamoja.
C. alienda kujisaidia mara kwa mara.
D. mwalimu alimwona amejikunyata darasani.

194. Shawe alikuwa na bahati kwani,
A. shida yake haikuwa hatari.
B. hakuwa na shida yoyote.
C. shida yake iligunduliwa mapema.
D. watu wote walimwombea.

195. Viungo vya mwili vilivyotajwa hulahta kazi gani?
A. Kusukuma damu mwilini.
B. Kusafisha damu.
C. Kuyeyusha chakula.
D. Kuhifadhi mkojo.

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 196 mpaka 200. Kwa kila swali umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Watu __196__ wanashiriki, michezo huwa na afya __197__. Jambo hili huwasaidia __198__ magonjwa __199__ kuhatarisha maisha yao. Hata hivyo, mtu __200__ mazoezi, huathirika kiafya.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 196. A. ambaye | B. ambapo | C. ambao | D. ambayo |
| 197. A. mzuri | B. njema | C. jema | D. mwema |
| 198. A. kuepuka | B. kuepusha | C. kuepukana | D. kuepukia |
| 199. A. zinazoweza | B. inayoweza | C. yanaweza | D. yanayoweza. |
| 200. A. akishiriki | B. alishiriki | C. anashiriki | D. asiposhiriki. |